OFISI YA RAIS - TAMISEMI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA

SHULE YA SEKONDARI KATUMA



S. L. P 438,
SUMBAWANGA.

ELIMU NI UKOMBOZI

TAREHE: **14/12/2020**

KUMB. NA/KASS/1/_____

JINA LA MWANAFUNZI _____

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KATUMA MWAKA 2021.**

1.0 UTANGULIZI

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule hii kidato cha kwanza mwaka 2021. Shule itafunguliwa tarehe 11 mwezi 01 mwaka 2021 tarehe ya mwisho kuripoti ni tarehe 18/01/2021 .

Pamoja na taarifa hii, ninapenda kukupongeza na kukukumbusha kwamba nafasi hii uliyoipata ni nadra na ya pekee pia ni nafasi ambayo vijana kama wewe wameikosa kwa sababu mbalimbali. Hivyo ninakukaribisha nikiamini kwamba utaitumia nafasi hii katika kujiendeleza mwenyewe na taifa zima.

Pamoja na barua hii nimeambatanisha;-

- Maagizo na mahitaji muhimu
- Fumu ya kukubali/kukataa nafasi uliyopata
- Fomu ya kuandikishwa shule na taarifa za wazazi/Walezi
- Fomu ya uchunguzi wa daktari (medical examination form)

Nakutakia maandalizi mema na kila la heri katika masomo ya sekondari.

Wako.

…….

AUGUSTINO GASPARY MSINIKWA

MKUU WA SHULE

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. Sare za shule
   Kwa wavulana, suruali mbali, rangi ya blue na kijivu, kwa wasichana sketi mbili rangi ya blue na kijivu ziwe ndefu hadi kwenye kisigino zikiwa fupi hazitakubaliwa, pia zisiwe na linda box. Kkipande cha kitambaa cha sample kimeambatanishwa.

2. Sare za michezo ni track suti ya blue.

3. Shati nyeupe mikono mifupi na tai ya blue au kijivu kwa wote.

4. Sweta rangi ya damu ya mzee.

5. Rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule (nyeupe) hii ni kwa wasichana wa kiislam.

6. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi, soksi nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana.

7. Picha (3) tatu paspoti size (upige ukiwa uimevaa shati jeupe).

8. Mchango wa chakula ni Tsh 70,000/= (elfu sabini) kwa mwaka. Pia unaweza kulipa kwa awamu mbili yaani kila muhula Tshs 35,000/=.

9. Vifaa vya usafi
   a. Ndoo moja mpya yenye ujazo wa lita kumi.
   b. Jembe kumbwa moja, liwe jipya.
   c. Fyekeo moja.
   d. Fagio moja aina ya chelewa.

10. Mti mmoja wa matunda (mwembe au mparachichi) uwe kwenye tube.

11. Madaftari makubwa 10 (counter book), biki, rula, mkebe mmoja na begi la kubebea vifaa hivyo.

12. Kamusi ya kiingereza - Kiswahili au Kiswahili - kiingereza.

13. Njoo na rimu 1 (karatasi) kwa ajili ya mazoezi darasani.

14. Sheria na kanuni za shule
    Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inatolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais OR-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake.

SHERIA ZA SHULE

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi, wageni na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulinagna na ratiba ya shule ni lazima.
3. Kushiriki kwa makini kuandaa maandalio.
4. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
6. Kutimiza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
9. Kutunza mali ya umma.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga.
3. Ubakaji.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocane, mirungi, kubeli na kadhalika.
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau bendera ya Taifa.
8. Kuwa mjaamzito/kupata mimba.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adshabu kwa makusudi.
13. Kuwa na simu ya mkononi.

FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI NA TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI.

A. TAARIFA ZA MWANAFUNZI

Jina kamili ulivyoandikishwa kwenye mtihani wa darasa la saba.

……..

Tarehe ya kuzaliwa …….

Dini ……

Mahali ulipozaliwa …….

Shule uliyohitimu shule ya msingi …….

B. TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI

1. Jina kamili ……
2. Wewe ni mzazi au mlezi …….
3. Kazi yako ……..
4. Dini ……
5. Wilaya ya nyumbani ……...
6. Maelezo mafupi kuhusu afya ya mwanafunzi ……..

   ……..
7. Anuani ya nyumbani ……..
8. Ninakiri kwamba taarifa zilizotolewa hapo juu ni kweli na sahihi.

……..

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI

FOMU YA KUKUBALI/KUTOKUBALI KUJIUNGA NA MASOMO YA SEKONDARI

Fomu hii ijazwe baada ya kusoma sheria za shule na fomu ya maagizo.

Nimezisoma sheria za shule kwa makini sana na ninaahidi kuzifuata.

Hivyo mimi …….. Nakubali/sikubali nafasi niliyopewa kujiunga na masomo ya sekondari kidato cha kwanza katika shule ya Katuma na ninahidi kufika shule na vitu vyote nilivyoagizwa.

……

Sahihi ya Mwanafunzi.

UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Nimesoma kwa makini na uangalifu sheria na maagizo ya kujiunga na elimu ya sekondari katika shue ya sekondari Katuma.

Hivyo ……. Nikiwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi …… nimekubaliana na ahadi zake na ninahidi kumsaidia kutekeleza yote na kutimiza mahitaji yake yote ya shule kwa wakati unaotakiwa.

……

Sahihi ya Mzazi/Mlezi

NB: Kutotekeleza maagizo kutasababisha mwanafunzi akose masomo na Mzazi/Mlezi kuchukuliwa hatua za kisheria.